

Wahandisi kutoka ZICTIA wakiendelea na kazi ya ukaguzi kwa ajili ya Kuufikisha Mkonga katika eneo la Uwanja wa Amani.

## MAFANIKIO

- Kutenga na kutangaza maeneo huru ya Uwekezaji wa TEHAMA Zanzibar (Zanzibar Digital Freezone) yaliyopo Fumba.
- Kutekeleza Mradi wa kujenga Kituo Mbadala Cha Kuhifadhia Taarifa (Tier 3 Data Center) katika maeneo ya Uwekezaji wa TEHAMA Fumba.
- Kufanikisha makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa kuweka Mkonga wa Kimataifa wa Baharini (International Gateway) na kujenga Mji wa TEHAMA (Cyber City).
- Kufikisha Mkonga wa Taifa katika kila Wilaya na kufikia zaid Asilimia 95% ya Taasisi za Serikali zilizounganishwa na Mkonga huo.
- Kuimarisha mfumo mzima wa Kituo Cha Taifa Cha Kuhifadhia Taarifa cha Serikali (Data Center) na kuwa kituo cha kisasa na cha kibiashara.
- Kuanza utekelezaji wa kupeleka huduma nafuu ya matumizi ya TEHAMA kwa wananchi kwa kuufikisha Mkonga Majumbani.

ZICTIA
SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR

**HUDUMA ZETU ZINAPATIKANA KUANZIA 02:00 ASUBUHI MPAKA 10:00 JIONI**

## KWA MAWASILIANO


### UNGUJA

+255 242235784

S.L.P 1823

info@zictia.go.tz, support@zictia.go.tz

www.zictia.go.tz

zictia

Mazizini, Zanzibar, Tanzania


### PEMBA

Chake Wesha Tibirinzi, Kusini Pemba, Zanzibartanzania.


Zanzibar Government Printing Press Agency



# ZICTIA
SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR




# RAMANI ZA MKONGA WA TAIFA WA MAWASILIANO

## UTANGULIZI

Shirika la mawasiliano zanzibar **(ZICTIA)** limeanzishwa mwaka **2023 kwa Sheria namba 4 ya mwaka 2023**, lengo kuu la shirika hilo ni kusimamia Miundombinu ya **TEHAMA**, Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Kuhifadhia Taarifa **(Data Center)** ili kuongeza mapato na kukuza uwekezaji katika sekta ya mawasiliano nchini.

## DIRA

Kuekeza Zaidi katika Miundombinu ya **TEHAMA** ambayo itaisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kurahisisha huduma za mawasiliano na kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

## DHAMIRA

Kuhakikisha Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali, zinaunganishwa na kutumia huduma zinazopatikana kupitia Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano, hii itasaidia katika upatikanaji wa haraka wa huduma zinazotokana na Mkonga huo.

Kutoa nafasi kwa vyombo na Taasisi Binafsi kujiunga na huduma za Mkonga, hii itasaidia katika kukuza Teknolojia ya Mawasiliano kwa haraka na kiurahisi zaidi.

## MAJUKUMU

Kwa mujibu wa Kifungu cha **7 (1) (a-p)** ya kuanzishwa kwa Shirika la Mawasilino Zanzibar, Shirika limeelezea kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuimarisha usalama,ulinzi wa mtandao na mazingira bora ya kiuchumi na kibiashara ya huduma za kitaifa za **TEHAMA** kupitia ushajihishaji wa usimamizi bora, matengenezo kama itakavyoamuliwa kwa mujibu wa sheria hii.
- Kusimamia na kuendeleza kituo kikuu cha taifa cha kuhifadhi taarifa Zanzibar.
- Kutoa ruhusa ya matumizi na uunganishwaji wa Miundombinu ya **TEHAMA** katika Taasisi zote za Serikali,watoa huduma za simu na mtandao au wateja wengine wowote.
- Kutoa msaada wa kiufundi kwa wateja wa Shirika.
- Kutoza ada kwa huduma zinazotolewa na Shirika.
- Kushajihisha uwekezaji wa ndani na nje katika huduma za **TEHAMA**.

## HUDUMA

- Huduma ya uwekaji wa vifaa vya elektoniki katika Miundombinu yetu kwa kitaalamu inajulikana kama **COLOCATION**.
- Huduma ya ukodishwaji wa seva kwa ajili ya uhifadhi wataarifa au mifumo ambayo kitaalamu inajulikana virtual mashine. Huduma hii humuwezesha mteja na taasisis za serikali kupatiwa sehemu ya seva zetu kulingana na mahitaji yao ili kuhifadhi taarifa zao na mifumo katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa **(Data center)** chenye kuzingatia usalama, unafuu, uendelevu na jumuishi. huduma hii humsaidia mteja huokoa gharama za kununua seva nzima pamoja na gharama za uendeshaji wa kifaa hicho.
- Huduma ya kuunganishwa kwa taasisis za serikali na wateja wa Taasisi Binafsi na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya huduma ya mitandao ya **INTERNET** na **INTRANET** yenye kasi kulingana na mahitaji ya mteja.
- Huduma ya kukodisha uwezo wa kupitisha mawasiliano/taarifa traffic kwa kitaalamu **CAPACITY LEASING** kwa Dar es salam Fumba na Tanga Pemba.
- Huduma ya kupitisha taarifa katika mitandao binafsi ulio ndani ya Miundombinu yetu **VPN** huduma hii huwezesha kuimarisha usalama wa Mawasiliano, taarifa na mifumo wa mteja.
- Huduma ya **IP MPLS**



Wahandisi kutoka **ZICTIA** wakiendelea na kazi katika Kituo cha Taifa cha kuhifadhia Taarifa **(Data Center)** Zanzibar.

## MALENGO NA MPANGO MKAKATI

**ZICTIA** imejiwekea malengo na mpango mkakati kama ifuatavyo;

- Kutoa huduma za Miundombinu ya **TEHAMA** yenye unafuu, uendelevu, usalama na jumuishi yenye kuwezesha kutoa huduma kwa Umma.
- Kuimarisha na kuendeleza Miundombinu ya **TEHAMA** na huduma zake.
- Kushajihisha na kuimarisha mchango wa Miundombinu ya **TEHEMA** kwa maendeleo ya Uchumi Zanzibar.
- Kufanya tathmini ya kijamii na mazingira kwa ajili ya kuhifadhi na kupata ufumbuzi wa athari zinazoweza kutokea katika Miundombinu ya **TEHAMA** kwa Umma.
- Uvumbuzi wa upanuzi wa Huduma zitokanazo na Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kadri ya uhitaji wa huduma husika kwa Umma.
- Kuhakikisha Taasisi za Serikali zinaunganishwa na Mkonga wa Mawasiliano ili kurahisisha na kuboresha upatikanaji wa huduma za Mawasiliano na kuokoa gharama kubwa ambazo zilikuwa ni mzigo kwa Serikali.